**TAARIFA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI MHESHIMIWA UMMY A. MWALIMU (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI ZA WILAYA, MIJI, MANISPAA NA MAJIJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

## 1.0 Utangulizi:

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inao utaratibu wa kutoa taarifa za **mapato ya ndani ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji na matumizi ya mapato hayo** kila robo mwaka ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri nchini. Taarifa hii ni ya robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/21, hivyo, imejumuisha taarifa ya mwaka wa fedha 2020/21.

Taarifa hii inaainisha ufanisi wa kila Halmashauri katika kukusanya mapato ya ndani kwa kulinganisha makisio idhinishwa. Uchambuzi wa matokeo umeandaliwa kwa kulinganisha aina za Halmashauri katika makundi na Kimkoa. Kadhalika, taarifa hii inaonesha mwenendo wa matumizi ya mapato ya ndani kwa kuainisha matumizi ya kawaida, matumizi ya miradi ya maendeleo ikiwemo asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

## 2.0 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri zilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 814.9** kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Halmashauri zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 757** ambayo ni **asilimia 93** ya makisio ya mwaka. Mapato halisi kwa mwaka wa fedha yameongezeka kwa **Shilingi bilioni 40** sawa na **asilimia 6** ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa mwaka wa fedha 2019/20 ambayo yalikua **Shilingi bilioni 717** kati ya bajeti ya **Shilingi bilioni 765.5.**

Uchambuzi wa taarifa kuhusu ufanisi wa Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, unaonesha kuwa Halmashauri **57** zimekusanya kwa **asilimia 100** au zaidi ya makisio yake ya mwaka, Halmashauri **90** zimekusanya kati ya **asilimia 80 hadi 99** na Halmashauri **37** zimekusanya kati ya **asilimia 50 hadi 79**. Ulinganisho wa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani unaonesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya **Nyang'hwale** imeongoza katika Halmashauri zote 184 kwa kukusanya **asilimia**

**163** ya makisio yake ya mwaka, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya **Mpimbwe asilimia 136** na Halmashauri ya Wilaya ya **Morogoro asilimia 133.** Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya **Mtama asilimia 51**, Halmashauri ya Wilaya ya **Serengeti asilimia 51** na Halmashauri ya Wilaya ya **Bumbuli asilimia 52,** Halmashauri hizi zimekuwa za mwisho katika ukusanyaji wa mapato ya ndani *(Kiambatisho Na. 1A)***.**

Katika kuzipima Halmashauri zote kwa kigezo cha wingi wa mapato (pato ghafi), Halmashauri ya **Jiji la Dar es Salaam** imekusanya mapato mengi zaidi kuliko Halmashauri zote kwa kukusanya **Shilingi bilioni 67.09** ikifuatiwa na Halmashauri ya **Manispaa ya Kinondoni bilioni 40.7** na **Halmashauri ya Jiji la Dodoma bilioni 38.4**. Aidha, Halmashauri **10** kati ya **184** zimekusanya kuanzia **Shilingi bilioni 10** na zaidi na Halmashauri **9** zimekusanya chini ya **Shilingi bilioni 1** *(Kiambatisho Na. 1B).*

Aidha, makusanyo Ki-Mikoa, **Mkoa wa Njombe** umeongoza kwa kukusanya **asilimia 113** ikifuatiwa na Mkoa wa **Geita asilimia 107, Mkoa wa Songwe asilimia 107** na **Mkoa wa Lindi** umekua wa mwisho kwa kukusanya **asilimia 78** ukifuatiwa na **Mkoa wa Simiyu asilimia 81** na Mkoa wa **Singida asilimia 82** *(Kiambatisho Na. 2).*

## 2.1 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa kuzingatia Aina ya Halmashauri:

### 2.1.1 Halmashauri za Majiji - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 6

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 **Halmashauri ya Jiji la Mbeya** imeongoza kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 102** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam asilimia 99** na **Halmashauri ya Jiji la Mwanza asilimia 92.** Aidha, **Halmashauri ya Jiji la Arusha** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **asilimia 80** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Jiji la Dodoma asilimia 82** na **Jiji la Tanga asilimia 88** *(Kiambatisho Na. 3A).*

### 2.1.2 Halmashauri za Manispaa - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 20

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 **Halmashauri ya Manispaa ya Kahama** imeongoza kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 109** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni asilimia 106** na **Halmashauri ya Manispaa ya Temeke asilimia 105.** Katika kundi hili **Halmashauri ya Manispaa ya Lindi** imekuwa ya mwisho ambapo imekusanya **asilimia 58** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Manispaa ya Tabora asilimia 76 na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji asilimia 78** *(Kiambatisho Na. 3B).*

### 2.1.3 Halmashauri za Miji - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 21

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 **Halmashauri ya Mji wa Njombe** imeongoza kwa kukusanya **asilimia 131** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Mji wa Kibaha asilimia 116** na **Halmashauri ya Mji wa Mafinga asilimia 108.** Aidha, **Halmashauri ya Mji wa Ifakara** imekuwa ya mwisho kwa kukusanya **asilimia 64** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Miji wa Korogwe asilimia 66** na **Halmashauri ya Mji wa Nanyamba asilimia 70** *(Kiambatisho Na. 3C).*

### 2.1.4 Halmashauri za Wilaya - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 137

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 **Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale** imeongoza kwa kukusanya **asilimia 163** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe asilimia 136** na **Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro asilimia 133**. Aidha, **Halmashauri ya Wilaya ya Mtama** na **Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti** zimekuwa za mwisho katika kundi hilo kwa kukusanya **asilimia 51** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli asilimia 52** *(Kiambatisho Na. 3D).*

## 3.0 Matumizi ya Mapato ya Ndani:

### 3.1 Matumizi katika Miradi ya Maendeleo

Uchambuzi wa taarifa za matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/21 unaonesha kuwa matumizi ya fedha za mapato ya ndani katika shughuli za miradi ya maendeleo Halmashauri zimetumia **Shilingi bilioni 279.7** sawa na **asilimia 92** ya fedha zilizopaswa kutumika kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni **Shilingi bilioni 303.6** ambazo ni **asilimia 40 au 60** ya mapato halisi yasiyolindwa. Halmashauri **37** zimetumia **asilimia 100** au zaidi ya kiasi kilichopaswa kutumika, Halmashauri **131** zimetumia kati ya **asilimia 50** na **99** ya kiasi kilichopaswa kutumika na Halmashauri **16** zimetumia chini ya **asilimia 50** ya kiasi kilichopaswa kutumika. Aidha taarifa zinaonesha kuwa Halmashauri ya **Wilaya ya Kondoa** imeongoza kwa kuchangia **asilimia 192.3** ikifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru asilimia 166** na **Halmashauri ya Wilaya ya Newala asilimia 155.** Aidha, **Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu** imekua ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 25.47** ikifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe asilimia 28 na Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli asilimia 28** *(Kiambatisho Na. 4).*

### 3.2 Mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Uchambuzi wa taarifa za matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/21 unaonesha kuwa Halmashauri zimechangia kiasi cha **Shilingi bilioni 53.8** kwenda kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni **asilimia 86** ya kiasi kilichopaswa kuchangiwa ambayo ni **Shilingi bilioni 62.7** ambayo ni **asilimia 10** ya mapato halisi ya vyanzo visivyolindwa kilichokusanywa katika kipindi hicho. Halmashauri **40** zimechangia **asilimia 100** au Zaidi, Halmashauri **120** zimechangia kati ya **asilimia 50 na 99** na Halmashauri **24** zimechangia chini ya **asilimia 50** kwenye Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Taarifa zinaonesha kuwa **Halmashauri ya Wilaya ya Chato**

imeongoza kwa kuchangia **asilimia 207** ikifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu asilimia 183** na **Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa asilimia 167.** Aidha, **Halmashauri ya Wilaya ya Chemba** imekua ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 13** ifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe asilimia 15** na **Halmashauri ya Mji wa Masasi asilimia 21** *(Kiambatisho Na.5).*

## 4.0 Changamoto Zilizobainika:

Katika kufuatilia usimamizi wa mapato ya ndani ya Halmashauri na matumizi yake, tumebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

4.1 Baadhi ya Halmashauri kutokuingiza taarifa za ukusanyaji mapato kwenye mfumo kwa wakati hivyo, kupelekea ugumu na ucheleweshaji wa uandaaji wa taarifa ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu Mapato na Matumizi;

4.2 Baadhi ya Halmashauri kuingiza mapato kwenye vifungu visivyo sahihi hivyo, kupelekea kufanya marekebisho na kuchelewesha uandaaji wa taarifa kutoka kwenye mfumo;

4.3 Baadhi ya Halmashauri kuchelewa kufanya usuluhishi wa taarifa za mapato kwenye mfumo wa Uhasibu hivyo, kuchelewesha uandaaji wa taarifa kutoka kwenye mfumo.

4.4 Baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani hivyo, kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii ikiwa ni pamoja na uchangiaji wa miradi ya maendeleo na mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

**Ili kukabiliana na changamoto hizi, tutahakikisha yafuatayo;**

a) Kwa mwaka wa fedha 2021/22; Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa zitahakikisha kazi ya uingizaji wa mapato pamoja na usuluhishi wa taarifa za fedha inafanyika kila mwezi ifikapo au kabla ya tarehe 15 baada ya mwezi husika kuisha;

b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa itaendelea kuzisimamia Halmashauri katika masuala ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya mifumo ili kuondoa mianya ya uvujaji wa mapato;

c) Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

d) Halmashauri zitaendelea kuhimizwa kuchangia miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria;

e) Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa taarifa ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

## 5.0 Maelekezo kwa Mikoa, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya:

### 5.1 Maelekezo kwa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya:

5.1.1 Halmashauri ziendelee kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani ambavyo haviitakuwa kero kwa wananchi ili kuongeza uwezo wa utoaji huduma kwa wananchi hususani huduma bora za Afya, Elimu na Miudombinu ya Barabara.

5.1.2 Halmashauri ziimarishe usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato ili kuondoa mianya ya uvujaji wa mapato. Kadri inavyowezekana kila chanzo kikusanywe kwa kutumia POS machine ili kudhibit upotevu wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

5.1.3 Halmashauri zihakikishe kuwa fedha za makusanyo ya ndani zinazokusanywa zinapelekwa benki ndani ya masaa 24 baada ya kuzikusanya. Ni marufuku na ni kosa la kisheria kwa Halmashauri kutumia fedha zilizokusanywa kabla ya kuzipeleka benki (fedha mbichi) kwa sababu yoyote ile.

5.1.4 Halmashauri zihakikishe zinapeleka na kutumia angalau **asilimia 40** ya mapato yaliyokusanywa (kwa Halmashauri zinazokusanya chini ya Shilingi bilioni 5 kwa mwaka) na **asilimia 60** (kwa Halmashauri zinazokusanya zaidi ya Shilingi bilioni 5 kwa mwaka) kwenye miradi ya maendeleo ili kutatua kero za wananchi hususan kuboresha huduma za Afya, Elimu na miundombinu ya barabara. Fedha hizi zitumike kwenye miradi yenye tija na inayogusa moja kwa moja wananchi na sio kugharamia semina, vikao, safari na mambo mengine yasiyogusa wanananchi moja kwa moja. Aidha kwa Halmashauri zenye makusanyo kuanzia **bilioni 5** na zaidi kwa mwaka, zihakikishe zinatumia angalau **asilimia 10** ya sehemu ya fedha zao za maendeleo kwenye uboreshaji wa Miundombinu ya barabara kupitia TARURA. Aidha, ninazitaka Halmashauri kuhakikisha fedha za mapato ya ndani zinatumika kutekeleza na kukamilisha miradi kwa **asilimia 100** ili wananchi waweze kuona faida za mapato ya ndani na hatimaye kuongeza mwamko wa ulipaji wa kodi na ushuru.

5.1.5 Halmashauri zihakikishe zinapeleka **asilimia 10** ya fedha za mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwenye shughuli zenye tija kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na ili kutekeleza hili, Halmashauri zihakikishe angalau asilimia 60 ya fedha za mikopo zinatolewa kwenye Vikundi hivi.

5.1.6 Halmashauri zihakikishe zinakamilisha miradi ambayo haijakamilika (viporo) kabla ya kuanzisha miradi mipya.

5.1.7 Halmashauri zitumie sehemu ya fedha za matumizi ya kawaida kutoka kwenye mapato ya ndani ili kulipa madeni na hatimaye kuondoa malimbikizo ya madeni yasiyokuwa na msingi.

5.1.8 Mabaraza ya Madiwani yahakikishe yanasimamia ipasavyo matumizi ya fedha za Halmashauri ili kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika. Aidha mabaraza ya madiwani yana wajibu wa kuhakisha fedha zinatumika kwenye miradi ya maendeleo yenye tija na manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

## 5.2 Maelekezo kwa Mikoa:

5.2.1 Sekretarieti za Mikoa zifanye ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na matumizi ya mapato hayo kwa Halmashauri zilizo ndani ya Mikoa yenu mara kwa mara ili kujiridhisha na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na matumizi yake na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Ofisi ya Rais – TAMISEMI kila robo mwaka kabla ya tarehe 20 baada ya robo husika kuisha. Aidha nina

5.2.2 Sekretarieti za Mikoa zifanye ufuatiliaji wa fedha za miradi inayotekelezwa kwa mapato ya ndani iliyopo kwenye Halmashauri zao ili kujiridhisha na ubora wa Miradi inayotekelezwa. Aidha Sekretariat zifanye ufuatiliaji wa kina wa miradi inayotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu na wadau wengine.

**Imetolewa na:**

Ummy A. Mwalimu (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI, OR – TAMISEMI**

**29 Julai, 2021**